

HALMASHAURI YA JIJI LA TANGA

Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi wa Jiji

Simu:

Mkurugenzi wa Jiji: 27 2643068

Idara zote: 27 2644530/3

Fax: 255 27 2644141/27 2647905

E-Mail: info@tangacc.go.tz



Barabara ya Hassani Ngwilizi

S. L. P. 178,

Tanzania.

Kumb.Na. TCC/S.20/57/C/193

17/08/2021

TANGAZO LA KAZI

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA JIJI LA TANGA ANAPENDA KUTANGAZA NAFASI ZA KAZI KWA WATANZANIA WOTE WENYE SIFA KAMA IFUATAVYO:-

1. Mtendaji wa Mtaa Daraja II Mshahara TGS B: Nafasi 3

Sifa za kuajiriwa:

Waombaji wawe na Elimu ya kidato cha IV/VI waliohitimu Astashahada (NTA Level 5) katika fani ya Utawala, Sheria, Elimu ya jamii (Sociology), Usimamizi wa Fedha (Finance Management), Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo.

Kazi na majukumu:

- i. Kusimamia ulinzi na Usalama wa raia na mali zao na kuwa mlinzi wa Amani katika Mtaa.
- ii. Katibu wa Kamati ya Maendeleo ya Mtaa
- iii. Kumwakilisha Mkurugenzi wa Halmashauri katika utekelezaji na usimamizi wa shughuli za maendeleo katika Mtaa
- iv. Kuandaa mpango kazi wa Maendeleo wa Mtaa na kuwasilisha kwa Mkurugenzi wa Halmashauri kuititia kwa Afisa Mtendaji Kata.
- v. Mtendaji Mkuu wa Mtaa na kiungo cha Uongozi kwa Idara zote kwenye Mtaa
- vi. Mratibu na msimamizi wa upangaji wa mipango shirkishi ya maendeleo ya Mtaa
- vii. Kusimamia utendaji kazi wa wataalamu na watendaji wa Mtaa

- viii. Kutafsiri na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni na miongozo ya Serikali katika Mtaa.

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIWA KWA WAOMBALI WOTE:

1. Muombaji awe Raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 hadi 45
2. Maombi yaambatanishwe na vivuli vya vyeti, picha moja ya paspoti saizi iliyopigwa hivi karibuni, maelezo binafsi (CV) ya muombaji na namba ya simu.
3. Watumishi waliowahi kuajiriwa Serikalini na kupata Cheki Namba hawataajiriwa tena bali wataajirwa baada ya kupata kibali cha Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.
4. Juu ya bahasha aandike kazi aliyoomba,
5. Transcript na provision result havipokelewi
6. Maombi yote yatumwe kwa:
Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji,
S.L.P. 178,
TANGA.
7. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 30/08/2021 saa 9.30 mchana.



Sipora J. Liana

**MKURUGENZI WA JIJI
MKURUGENZI WA JIJI
TANGA**